**RAIS SAMIA ASHIRIKI MKUTANO WA 38 WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA UMOJA WA AFRIKA (AFRICAN UNION)**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akishiriki Mkutano wa Kawaida wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika kwenye ukumbi wa Nelson Mandela uliopo Makao Makuu ya Umoja huo, Addis Ababa nchini Ethiopia tarehe 15 Februari, 2025. Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali ulitanguliwa na Kikao cha 49 cha Wawakilishi wa Kudumu wa Umoja wa Afrika kilichofanyika tarehe 14 Januari hadi 10 Februari 2025 na Kikao cha Baraza la Mawaziri la Umoja huo kilichofanyika tarehe 12 na 13 Februari 2025. Pamoja na masuala mengine mkutano huo umetangaza Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Afrika kwa Mwaka 2025, inayojumuisha nchi moja kutoka kanda tano za Umoja wa Afrika. Mwenyekiti Mpya ametoka kanda ya Kusini – Jamhuri ya Angola; Makamu Mwenyekiti wa Kwanza ametoka Kanda ya Afrika ya Kati – Jamhuri ya Burundi; Makamu Mwenyekiti wa Pili ametoka Kanda ya Magharibi – Jamhuri ya Ghana; Makamu Mwenyekiti wa Tatu ametoka Kanda ya Mashariki - Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu ambaye ni Mwenyekiti aliyemaliza muda wake kutoka Kanda ya Kaskazini - Mauritania.